# TRIAL SERIES

# STD 6 - TERM III

# KISWAHILI

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 10. Kwa kila nafasi umepewa maneno hapo chini.**

**Chagua maneno yafaayo kujazia nafasi zilizo wazi**

Watu __1___ hupenda __2___ kushindana __3___ ya kuwa na sababu za __4___. Hii ni tabia __5___ na __6___ __7___. Hakuna __8____ __9___ ya kuwa __10___.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | nyingine | mwingine | wengine | zingine |
| 2. | tu | lau | hivi | tena |
| 3. | hata | bali | maana | bila |
| 4. | kutishana | kutoshea | kutosheleza | kutosha |
| 5. | zao | wao | yao | [illegible] |
| 6. | ndivyo | ndiyo | ndizo | ndio |
| 7. | walinukulia | walivyokulia | walizokulia | walipokulia |
| 8. | zaidi | desturi | maisha | namna |
| 9. | wowote | zozote | yeyote | yoyote |
| 10. | badili | badali | badilishana | badilisha |

Sote tulikuwa hatuna __11___ ila kujikaza __12___ kupambana na jangili lililotuvamia. __13___ lilikuwa jitu lisilokuwa na huruma. Ingawa kila mmoja wetu __14___ kulala chini bado lilikuwa __15___ kama radi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | budi | bundi | shakà | shauku |
| 12. | kikwetu | kinguru | kisabuni | kibolela |
| 13. | afan alek! | kefu! | ingawa! | la haula! |
| 14. | alilazimishwa | alilazimisha | alilazimu | alilazimiana |
| 15. | likinguruma | likitetea | likisema | likidokeza |

**Kutoka swali la 16-30 chagua jibu lililo sahihi**

16. Neno 'maktaba' liko katika ngeli ya ______

A. li - ya B. u - u

C. ya - ya D. i - zi

17. Umepoteza funguo ________?

A. ngapi B. mangapi

C. vingapo D. mingapi

18. Mbwa ______ ndiye anayebweka usiku kucha.

A. yuyu huyu B. wuwu huyu

C. wuwu yuyu D. wuyu huyu

19. **Kikundi kipi cha maneno kimekosewa?**

A. Hayati, marehemu, mstahiki

B. Tunutu, kupe, kiluwiluwi

C. Kiroboto, kunguni, nyungunyungu

D. Umbu, mpwa, ami

20. ______ macho haambiwi tazama.

A. Wenye B. Mwenye

C. Yenye D. Lenye

21. Akisami hii. $^{1}/_{8}$ huitwa__________

A. sudusi B. subui

C. tusui D. thumni

22. Tarakimu ambayo hubadilika kulingana na ngeli ni

A. sita B. nane

C. saba D. tisa

23. ______ ni nafasi iliyotengenezwa ukutani kuwekea vitu.

A. Shubaka B. Rafu

C. Shufaka D. Shuduza

24. Ujeuri ________ unao unakuchongea.

A. ambayo B. ambaye

C. ambao D. ambalo

25. Neno gani si kisawe cha 'nia'?

A. Wazo B. Lengo

C. Shabaha D. Madhumuni

26. Maana ya 'alinilimisha' ni ________

A. alinifanya nimlimie

B. mimi nilimlimia naye akanilimia

C. yeye alinilimia baada ya mimi kumlimia

D. alinilimia shamba langu

27. Nomino ambata ambayo si sahihi ni ________

A. kiazichege B. kiazishume

C. kiazikitamu D. kiazi cherema

28. Tunasema halaiki ya watu, pia ______ wa magari.

A. umati B. mlolongo

C. shehena D. jamii

29. **Chagua sentensi sahihi kisarufi.**

A. Huko ndipo kwenye giza

B. Humo ndiko kwenye giza

C. Hao ndiwo wanaokupoteza

D. Hayo ndiyo malengo

30. Watu wote walishiba sana. Maneno yaliyopigwa mstari ni __________

A. kivumishi cha sifa na kielezi

B. kielezi na kivumishi cha pekee

C. kiambishi na kielezi

D. kivumishi cha pekee na kielezi

**Soma mkasa huu kisha uchague majibu sahihi zaidi ya maswali 31-40**

Kondoo alikuwa akila nyasi kama ada na desturi yake. Mchungaji wake alikuwa mbali kiasi akishughulikia mifugo wengine. Muda mrefu haukupita akatokea mbweha. Akamkaribia kondoo huyo aliyekuwa mbali na wenziwe. Kondoo huyo alikuwa na mafuta mengi na kunona bila kiasi.

Mbweha alitaka kumshambulia kondoo papo hapo. Kondoo akamwambia, "mbona mwenzangu una pupa hivyo. Mimi nimeletwa hapa kando na mchungaji wangu ili upate kunila. Mimi na yeye ni pamba na moto. Hilo usilitie shaka. Hunioni niko mbali na wenzangu. Lakini kabla hujanila nataka nikuimbie wimbo mtamu wa kuburudisha roho yako. Mimi na wewe hatuteti.

Yule mbweha akafurahi mno. Akaona siku hiyo angekula nyama ya kondoo ya hali ya juu. Tena alikuwa peke yake. Kwa hivyo angemla shibe yake.

Kondoo akaimba kwa kelele mbweha akaonyesha furaha yake kuimbiwa. Mchungaji aliposikia sauti ya kondoo wake, akajua kuwa kondoo yule yuko hatarini. Akaja haraka haraka kwa kondoo wake mkuki mkononi. Mbweha kumwona mchungaji jinsi alivyokuwa anakuja akatoweka bila ya kujulikana alikokwenda kujificha.

31. Mwili wa kondoo kidesturi hufunikwa kwa ______

A. sufu B. sufi

C. nundu D. magamba

32. Wahusika katika kifungu hiki ni _______

A. wawili B. watatu

C. wanne D. mmoja

33. Mchungaji alikuwa ________

A. karibu na kondoo wake

B. karibu sana na mbweha

C. kando ya kondoo mmoja

D. anatafuta mbweha kumuua

34. Mbweha alipomwona kondoo yule aliyekuwa peke yake ______

A. aliudhika B. alihuzunika

C. alishtuka D. alishukuru

35. **Maliza methali hii.** Mwenye pupa ________

A. ndiye mla nyama B. hadiriki kula tamu

C. ni mwenye njaa nyingi D. huwahi kilichoko

36. Maana ya mimi na yeye ni pamba na moto ni ______

A. hatusikizani B. hatuachani

C. hatujuani D. hatuteti

37. Kondoo alitaka kuimba kwa sababu ________

A. mbweha hupenda kuimba

B. kondoo lazima waimbe kabla ya kuchinjwa

C. kondoo alikuwa na sauti nzuri sana

D. alitaka kumjulisha mchungaji wake

38. Mbweha alikimbia kwa sababu ________

A. alishindwa kumla kondoo

B. njaa ilimzidi hakuweza kustahimili

C. alimwogopa mchungaji aliyekuja haraka

D. aliitwa na wenzake huko tokomiani

39. Kilichomtia hatarini kondoo ni ________

A. kuimba kwake

B. kujitenga kwake

C. kunona kwake

D. kuteta na mchungaji wake

40. Kichwa kinachofaa zaidi kwa mkasa huu ni ____

A. Kufa kikondoo ndiko kufa kiungwana

B. Akili ni nywele kila mtu ana zake

C. Mbwa hafi akiona ufuko

D. Siku njema huonekana asubuhi

**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali 41 - 50**

Katika kijiji kimoja cha mlima Kenya kulikuwa na mtoto mmoja wa kike. Mtoto huyu alikuwa maskini sana. Alikuwa na huruma na bidii kubwa. Baba yake alikuwa akiumwa kitandani na kupotewa na uwezo wa kufanya kazi. Mtoto huyo aliyasukuma maisha ya nyumbani kwa kuuza kuni tu. Kila siku alirauka mapema na kwenda kukata kuni mlimani.

Iliondokea siku moja kama kawaida yule mtoto alichukua shoka akaelekea mlimani kukata kuni ili apate pesa za kumtibu baba yake. Mtoto huyu alizungukazunguka mlimani kwa muda mrefu mwisho akaona mti mmoja mkubwa wenye matawi yaliyoshonana kando ya mto mdogo.

Akauendea na kuanza kuukata kwa shoka lake. Alipokaribia kuuangusha mti huo mkubwa kwa ghafla shoka lake lilimponyoka mkononi likaingia mtoni. Alihuzunika sana. Haukupita muda maji ya mto yakaanza kujaa. Kichwa cha mzee mmoja kikajitokeza kutoka mawimbini. Kuona vile, mtoto aligutuka na kuanguka chini huku rinda lake likipasuliwa na matawi.

41. Maana ya neno alirauka ni ________

A. alilala B. alikula

C. aliamka D. aliona

42. Kulingana na habari hii, mzee aliyetajwa alikuwa

A. tajiri B. maskini

C. mkulima D. mwalimu

43. Mtoto hangeweza kupata riziki yake bila ____

A. kulima B. kuomba

C. kukata kuni D. kuomba omba

44. Mtoto huyu alitumia kifaa kipi kwa kazi yake?

A upanga B. utu

C. upole D. shoka

45. Mtoto aliona uchungu wakati ____

A. alipoteza shoka B. alikosa kuni

C. babake aliaga D. aliona kichwa

46. Baba mtoto alikuwa kitandani kwa sababu ya ____

A. kukosa shoka B. umaskini

C. ugonjwa D. utajiri

47. Kilichomshtua mtoto ni ________

A. mawimbi B. maji

C. kupotea kwa shoka D. kichwa cha mzee

48. Mtoto aliyetajwa alikuwa ________

A. na tabia nzuri B. mkorofi

C. mtundu D. tajiri

49. Umaskini si ________

A. ugonjwa B. kilema

C. ulemavu D. uzee

50. Kwa nini lile shoka likamponyoka kutoka mkononi mwa msichana yule?

A. kwa woga

B. kwa ushujaa wa kukata kuni

C. kwa sababu ya uchovu

D. kutokea kwa yule mzee kutoka mtoni